NAMBARI YA UAMUZI. ____20-159_____

Uamuzi wa Ahadi za Kwanza za Baraza zinazoshughulikia Vuguvugu la Maisha ya Watu Weusi ni Muhimu na Ubaguzi wa Rangi wa Kimfumo kufuatia kuuawa kwa George Floyd na Polisi wa Minneapolis na miito ya kuchukua hatua kutoka kwa wenyeji na waandamaji.

Kwa kuzingatia kuwa maandamano yametanda kote nchini na Iowa City kutokana na kuuawa kwa George Floyd na polisi wa Minneapolis; na

Kwa kuzingatia kuwa Jiji la Iowa City linaunga mkono kwa dhati haki muhimu ya kikatiba ya haki ya kujieleza na kukusanyika, jinsi inavyotekelezwa katika maandamano ya amani; na

Kwa kuzingatia kuwa wenyeji na waandamaji wanasisitiza kuwa Jiji na Baraza la Jiji lichukue hatua ili kushughulikia vuguvugu la Maisha ya Watu Weusi ni Muhimu na Ubaguzi wa Rangi wa Kimfumo; na

Kwa kuzingatia kuwa ubaguzi wa rangi wa kimfumo umekithiri zaidi katika mfumo wa nchi na jiji letu hivi kwamba juhudi pana na za kina zitahitajika; na

Kwa kuzingatia kuwa Baraza la Jiji limejitolea kutekeleza juhudi hizo na ni kwa ajili ya masilahi bora zaidi ya Jiji la Iowa City na wakazi wake; na

Kwa kuzingatia kuwa Baraza la Jiji lingependa kuanza kutekeleza ahadi zake za kwanza kwa vuguvugu la Maisha ya Watu Weusi ni Muhimu.

Kwa hivyo, sasa, Baraza la Jiji la Jiji la Iowa City, Iowa, limeamua kuwa:

Baraza linaahidi kutekeleza juhudi pana na za kina ili kushughulikia vuguvugu la Maisha ya Watu Weusi ni Muhimu na ubaguzi wa rangi wa kimfumo, ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

1. Kubuni mpango wa mwanzo wa kuweka mpangilio mpya wa Idara ya Polisi ya Iowa City (ICPD) ili kufanya polisi wafahamikiane na wenyeji, ikiwa ni pamoja na kupunguza hali ya umma kutegemea zaidi polisi katika hali zisizo za vurugu kupitia kutumia wataalamu ambao hawajajihami na kuzingatia mipango ya polisi kufahamikiana na wenyeji katika miji mingine, ikiwa ni pamoja na Minneapolis, MN, Camden, NJ, Los Angeles, CA na San Francisco, CA kufikia tarehe 15 Desemba 2020; na

2. Kutenga fedha za Jiji za kiasi cha $1,000,000 wakati wa Mwaka wa Bajeti kuanzia tarehe 1 Julai 2020 kwa juhudi za kuendeleza usawa wa rangi na haki ya kijamii, ikiwa ni pamoja na kupanua mpango wa Ushirikishaji wa Watu Maalum [SPI], kubuni mpango mpya mkubwa wa nyumba za bei nafuu, ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba mjini na mitaa ya karibu, kuunga mkono juhudi zinazotarajiwa kubainishwa za Tume ya Ukweli na Upatanishi na kufanya kipindi cha kazi ya Baraza mnamo au kabla ya tarehe 1 Agosti 2020 ili kushughulikia utengaji mahususi; na,

3. Kuendeleza juhudi za Jiji za usawa wa rangi na haki ya kijamii, ikiwa ni pamoja na kupanua juhudi za kuongeza idadi ya walio wachache wanaoajiriwa na Jiji ikiwa ni pamoja na kuondoa vizuizi vya kutuma maombi ya kazi, kuongeza nyenzo zilizotengwa kwa ajili ya juhudi hizo jinsi inavyohitajika ili kuwapa mafunzo wafanyakazi wote wa jiji kwa njia bora na kuratibu na kuripoti kuhusu matumizi ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya usawa wa rangi na haki ya kijamii; na,

4. Kufikia tarehe 1 Agosti 2020, kupokea ripoti kutoka kwa Msimamizi wa Jiji kuhusu kushiriki kwa ICDP katika matumizi ya gesi na magruneti ya kutoa mwangaza mwingi wakati wa maandamano Iowa City tarehe 3 Juni 2020; na,

5. Kufikia tarehe 1 Oktoba 2020, kubuni Tume ya Ukweli na Upatanishi ili kutoa ushahidi kuhusu ukweli wa kutokuwepo kwa usawa wa rangi Iowa City na kutekeleza haki ya urejesho, kupitia ukusanyaji wa ushahidi na maoni ya umma na kazi kama hiyo ijumuishe mapendekezo kwa Baraza kuhusu mpango wa kutenga na/au kubadilisha majina ya maeneo ya umma na/au haki za njia ya kuheshimu vuguvugu la Maisha ya Watu Weusi ni Muhimu; na,

6. Kufanya kiwe kipaumbele cha 2021 cha sheria ya Baraza la Jiji ya kutetea na kuunga mkono ujumbe wetu wa jimbo katika kutekeleza mageuzi ya haki za uhalifu, kuondoa vita dhidi ya dawa za kulevya na kufanya mabadiliko kwenye sheria ya jimbo ambayo inawezesha mpango wa Jiji wa kuweka mpangilio mpya wa idara ya polisi, kuimarisha mamlaka ya Bodi ya Jamii ya Ukaguzi wa Polisi (CPRB) na kupunguza tabia zisizofaa za walio wachache, ikiwa ni pamoja na kuunga mkono sheria ya jimbo ya kutochukua sheria za kihalifu dhidi ya kiasi kidogo cha bangi; na,

7. Kuendelea kutumia zana za usawa wa rangi na idara za jiji na kuendeleza mafunzo kama hayo kwa Baraza la Jiji na kushirikiana na washirika wetu wa biashara za eneo ili kuelimisha na kufunza wanabiashara kuhusu kutumia zana za usawa wa rangi; na,

8. Kuomba na kupokea ripoti na mapendekezo kutoka kwa CPRB kufikia tarehe 1 Januari 2021, kwa kushauriana na mwanasheria itakayomchagua, kuhusiana na mabadiliko kwenye sheria ya CPRB ambayo inaimarisha uwezo wake wa kutoa maarifa kwa umma kuhusu ICPD, ikiwa ni pamoja na yale yanayoshughulikia ushahidi wa kushawishi wa polisi na ripoti ijumuishe muhtasari wa mbinu zinazokubalika na zinazokataliwa na CPRB, iwe ni kwa ajili sababu za kisheria au za sera; na,

9. Kuelekeza wafanyakazi kutoa muhtasari wa kina wa matumizi ya fedha za bajeti ya polisi kwenye tovuti ya Jiji; na,

10. Kutuma barua iliyoambatishwa kama Ushahidi wa “A” kwa Liwali wa Kaunti ya Johnson inayounga mkono kuacha kutumika kwa gari la MRAP (Mine Resistant Ambush Protected) na kupata ripoti kutoka kwa wafanyakazi wa jiji kuhusu silaha za kiwango cha kijeshi zilizo katika orodha ya ICPD na mikataba ya nchi ambayo inatoa usaidizi kwa idara ya polisi; na,

11. Kumwelekeza Msimamizi wa Jiji kupiga marufuku moja kwa moja matumizi yoyote ya kumbana mtu shingo au njia nyingine yoyote ambayo inasimamisha mzunguko wa damu au kuingia kwa hewa mwilini katika sheria za jumla za ICPD; na,

12. Kumwelekeza Msimamizi wa Jiji kuhakikisha kuwa desturi na sera za ICPD zinazohusiana na kuajiri polisi zinalingana na malengo yaliyotolewa hivi majuzi ya Iowa House File 2647 ili kuhakikisha kuwa poilisi wanaofanya kazi Iowa hawajatekeleza kosa lolote kubwa, jinsi inavyobainishwa.; na,

13. Kumwelekeza Msimamizi wa Jiji kukagua mifumo na mbinu za kuripoti zinazotumika katika ICPD ili kutathmini iwapo zinatii sheria za ICPD za Kamera Zinazovaliwa Mwilini na sheria ya jumla ya Rekoda za Ndani ya Gari, kuhakikisha kuwa mifumo kama hiyo inatii kikamilifu sheria ya jumla, kuikagua jinsi inavyohitajika ili kutimiza lengo hilo, kujumuisha athari kamili za kutotii sheria na kuripoti kwa Baraza baada ya kukamilisha ukaguzi.; na,

14. Kumwelekeza Msimamizi wa Jiji kukagua sheria za jumla za ICPD ili kuhitaji polisi waingilie kati na kukomesha matumizi ya nguvu kupita kiasi ya polisi wengine na kuripoti tukio moja kwa moja kwa msimamizi na kuweka makubaliano ya uelewano na mashirika mengine ya eneo ya kutekeleza sheria kuhusu uingiliaji kati kama huo wakati nguvu kupita kiasi inatumika na polisi wa shirika lingine kama ile ambayo inajadiliwa kwa sasa na kusambazwa miongoni mwa mashirika ya eneo ya kutekeleza sheria iliyoambatishwa kama Ushahidi wa “B”; na,

15. Kuomba na kupokea na mapendekezo kutoka kwa Kamati ya Jiji ya Ushauri wa Sanaa ya Umma, baada ya kupokea maoni na kushauriana na wasanii Weusi wa eneo kuhusu mbinu ambazo Tume inapaswa kuzingatia ili kutoa fursa kwa maonyesho ya kisanaa na vuguvugu la Maisha ya Watu Weusi ni Muhimu na jamii za watu weupe, ikiwa ni pamoja na sanaa za kuona pamoja na tamasha la umma lililotengwa kwa ajili ya kusherehekea utamaduni wa Watu Weusi.

16. Kupiga marufuku matumizi ya vitoa machozi, risasi bandia na magruneti ya kutoa mwangaza mkali dhidi ya maandamano ya amani.

17. Kuanzia mwaka wa 2021, sherehe za maadhimisho ya ukombozi wa watumwa nchini Marekani, tarehe 19 Juni, itakuwa sikukuu ya jiji na itachukua nafasi ya sherehe ya jiji iliyopo.

Umepitishwa na kuidhinishwa siku hii ya tarehe 16 Juni 2020.

_____
Meya

Umeidhinishwa na:

Shahidi: _____ _____
Karani wa Jiji Ofisi ya Mwanasheria wa Jiji (17/06/2020)

Nambari ya Uamuzi. ___20-159____
Ukurasa wa 2

Ulipendekezwa na _____ na kuungwa mkono na _____ Uamuzi uanze kutumika na baada ya kuita orodha ya majina ya waliopo, kulikuwa na:

Wanaounga Mkono:	Wanaopinga:	Ambao Hawakuhudhuria:
__X____	_____	_____ Bergus
__X____	_____	_____ Mims
__X_____	_____	_____ Salih
__X____	_____	_____ Taylor
__X____	_____	_____ Teague
__X___	_____	_____ Thomas
__X____	_____	_____ Weiner

USHAHIDI WA A

JIJI LA IOWA CITY
410 East Washington Street
Iowa City, Iowa 55240-1826
(319) 356-5000
(319) 356-5009 FAKSI
www.icgov.org

Tarehe 17 Juni 2020

Lonny Pulkrabek
Liwali wa Kaunti ya Johnson
S.L.P 2540
511 S. Capitol Street
Iowa City, IA 52244

Mpendwa Liwali Pulkrabek,

Kwa niaba ya Baraza la Jiji la Iowa City, ninaandika ili kuomba kuwa ofisi ya Liwali iache kutumia gari la MRAP (Mine-Resistant Ambush Protected). Gari la kiwango cha kijeshi lililobuniwa kutumika katika maeneo ya vita halifai kutumika na shirika la eneo la kutekeleza sheria. Hali hii inadunisha imani ya umma kwa mashirika ya utekelezaji wa sheria na hivyo basi kuathiri lengo la kudumisha usalama wa jamii

Asante kwa kuelewa.

Wako mwaminifu,

Bruce Teague, Meya
Jiji la Iowa City

USHAHIDI WA B

MAKUBALIANO YA UELEWANO

Tarehe: Juni 10 2020

MAKUBALIANO haya ya UELEWANO yamewekwa kati ya Idara ya Liwali ya Kaunti ya Johnson, Idara ya Polisi ya Iowa City, Idara ya Usalama wa Umma ya Chuo Kikuu cha Iowa, Idara ya Polisi ya Coralville, Idara ya Polisi ya North Liberty na Idara ya Polisi ya University Heights ili kuwapa mamlaka polisi wetu wa kutekeleza sheria kutoka katika kila mojawapo ya eneo la mamlaka kuingilia kati iwapo watashuhudia matumizi ya nguvu kupita kiasi.

WAJIBU WA KUINGILIA KATI

Polisi yeyote wa kutekeleza sheria anayeshuhudia polisi mwingine wa kutekeleza sheria akitumia nguvu kupita kiasi ambayo haifai kutumika kulingana na hali iliyopo atakuwa na uwezo iwapo anaweza kufanya hivyo, kusihi ili kuzuia matumizi ya nguvu kupita kiasi.

Polisi na manaibu wao walioapishwa wanapaswa kulinda umma na wafanyakazi wengine bila kujali kazi, cheo au shirika la mwanachama na wanapaswa kuingilia kati kimwili na kwa maneno kwa njia salama.

Polisi wa kutekeleza sheria anayeshuhudia mfanyakazi mwingine akitumia nguvu kupita kiasi kuliko jinsi inavyoruhusiwa kisheria anapaswa kuripoti haraka iwezekanavyo hali hii kwa msimamizi.

Tunakubali na kuwajibu kwa jamii tunazohudumia.

Ni mimi wako,

_____
Bill Campbell, Mkuu wa Polisi wa Iowa City

_____
Scott Beckner, Mkurugenzi wa Usalama wa Umma wa Chuo Kikuu cha lowa

_____
Lonny Pulkrabek, Liwali wa Kaunti ya Johnson

_____
Shane Kron, Mkuu wa Polisi wa Coralville

_____
Diane Venenga, Mkuu wa Polisi wa North Liberty

_____
Troy Kelsay, Mkuu wa Polisi wa University Heights

JIJI LA IOWA CITY
410 East Washington Street
Iowa City, Iowa 55240-1826
(319) 356-5000
(319) 356-5009 FAKSI
www.icgov.org

Tarehe 17 Juni 2020

Janet Lyness
Mwanasheria wa Kaunti ya Johnson
417 S. Clinton Street
Iowa City, IA 52240

Mpendwa mwanasheria wa Kaunti Lyness,

Kwa niaba ya Baraza la Jiji na kwa mujibu wa mjadala uliopitishwa na Baraza la Jiji katika Mkutano wake Maalum wa Baraza mnamo tarehe 16 Juni 2020 ili kujadili Maisha ya Wetu Weusi ni Muhimu/Ubaguzi wa Rangi wa Kimfumo/Sera za Polisi, ninaomba kuwa kesi zote unazoshughulikia dhidi ya waandamaji wa Maisha ya Watu Weusi ni Muhimu zifutiliwe mbali.
Nimeambatisha muhtasari uliotolewa kwa Baraza na idara ya polisi wa maandamano na kesi zinazohusiana na trafiki zilizowasilishwa na ICPD kati ya tarehe 30/05/2020 na tarehe 09/6/2020 zinazokaribiana na maeneo ya maandamano, tarehe na saa.

Asante kwa kuelewa.

Wako mwaminifu,

Bruce Teague, Meya
Jiji la Iowa City

Viambatisho.

Tarehe/Saa (24HRS)	Eneo	Jiji la Makazi ya Mshitakiwa	MAKOSA	Ushahidi wa Polisi	KUTIWA MBARONI	ALIKAMATWA KISHERIA?
20200530 1:55	S CAPITOL ST/ COURT ST	GARNER, IA	KUENDESHA GARI UKIWA UMEKUNYWA POMBE AU KUTUMIA DAWA NYINGINE - INASUBIRI MATOKEO	HAPANA	inasubiri matokeo	HAPANA
20200530 23:17	E BURLINGTON ST/JOHNSON ST	NORTH LIBERTY, IA	KUENDESHA GARI KWA KASI YA JUU	NDIYO	HAPANA	HAPANA
20200605 21:45	E BURLINGTON ST/S SUMMIT ST	IOWA CITY, IA	KUENDESHA GARI UKIWA UMEPIGWA MARUFUKU	HAPANA	NDIYO	HAPANA
20200606 19:46	E COLLEGE ST/ S VAN BUREN ST	MOUNT PLEASANT, IA	ISHARA YA KUSIMAMA	NDIYO	HAPANA	HAPANA
20200606 20:30	HWY 1 W/MILLER AVE	IOWA CITY, IA	KASI	NDIYO	HAPANA	HAPANA
20200607 00:55	410 E WASHINGTON ST	CEDAR RAPIDS, IA	KUENDESHA GARI UKIWA UMEKUNYWA POMBE AU KUTUMIA DAWA NYINGINE, PCS BANGI, KUMILIKI BUNDUKI UKIWA UMEKUNYWA POMBE AU KUTUMIA DAWA NYINGINE	NDIYO	NDIYO	HAPANA
20200607 1:31	S GILBERT ST/ E COLLEGE ST	IOWA CITY, IA	KUKIUKA IDHINI YA MAAGIZO, KUSHINDWA KUTOA UTHIBITISHO WA DHIMA YA	NDIYO	HAPANA	NDIYO
20200607 01:33	HWY 1 W/ ORCHARD ST	IOWA CITY, IA	NAMBARI YA USAJILI WA GARI	NDIYO	HAPANA	HAPANA
20200608 18:55	E BURLINGTON ST/S DUBUQUE ST	IOWA CITY, IA	HAKUNA LESENI YA DEREVA, KUSHINDWA KUTOA UTHIBITISHO WA DHIMA YA KIFEDHA, KUSHINDWA KUONYESHA NAMBARI YA USAJILI WA GARI, KUTOTUMIA	NDIYO	HAPANA	NDIYO

			VIZURI MIKONDO YA BARABARA			
20200608 19:51	E MARKET ST/LINN ST	IOWA CITY, IA	NAMBARI YA USAJILI WA GARI AMBAYO MUDA WAKE WA KUTUMIKA UMEKWISHA	NDIYO	HAPANA	HAPANA
20200609 00:09	200 S CLINTON ST	IOWA CITY, IA	KUENDESHA GARI UKIWA UMEKUNYWA POMBE AU KUTUMIA DAWA NYINGINE	HAPANA	NDIYO	HAPANA
20200609 00:47	E COURT ST/ S GILBERT ST	WHEATON, IL	KUMILIKI VIFAA VYA DAWA ZA KULEVYA	HAPANA	NDIYO-imethibitishwa na kutolewa	HAPANA
20200609 00:47	E COURT ST/ S GILBERT ST	IOWA CITY, IA	KUMILIKI KITAMBULISHO KISICHO CHA KWELI, KUMILIKI VIFAA VYA DAWA ZA KULEVYA	HAPANA	NDIYO-imethibitishwa na kutolewa	HAPANA
20200603 22:45	DUBUQUE/ FOSTER	IOWA CITY, IA	TABIA ISIYOFAA, MKUTANO WA KINYUME CHA SHERIA	HAPANA	NDIYO	HAPANA
20200603 23:45	DUBUQUE/ MEADOW RIDGE LANE	IOWA CITY, IA	MKUTANO WA KINYUME CHA SHERIA, KUKATAA KUTAWANYIKA	HAPANA	NDIYO	HAPANA